Kichwa cha Sera:	Sera ya Punguzo la Wagonjwa Wasio na Bima – Idara ya Usimamizi wa Mapato	Kitambulisho cha Sera:	181
Maneno Msingi	**kifedha, msaada, asiye na bima, punguzo, mgonjwa**		
Idara:	**Idara ya Usimamizi wa Mapato (RMD)**		

I. Kusudi la Sera

Inahakikisha kwamba wagonjwa wasio na bima hawatozwi zaidi ya kiasi kinachotozwa kwa wale walio na bima zinazofadhili huduma hizo.

Sera hii inazingatia NH RSA 151:12-b, Kanuni ya Mapato ya Ndani Sehemu ya 501(r) na Sheria ya Ulinzi wa Mgonjwa na Huduma Nafuu ya mwaka 2009 na itakuwa inabadilishwa kwa vipindi kama inavyotakiwa ili kuzingatia vigezo.

II. Upeo wa Sera

Kwa makusudi ya sera hii “punguzo lisilo na bima” linamaanisha huduma za afya zinazotolewa Dartmouth-Hitchcock Health (D-HH) kwa wagonjwa wasio na bima au kwa huduma ambazo kwa ujumla zinafadhiliwa na bima lakini hazifadhiliwi kwa baadhi ya huduma.

III. Ufafanuzi

Bima ya pamoja: Asilimia ya gharama za huduma za afya ambazo kuna ushiriki wa pamoja kati ya kampuni ya bima na mpokeaji wa bima kama inavyoelezwa na sera ya mpokeaji wa bima.

Malipo ya Pamoja: Ada isiyobadilika ambayo wanachama wa mpango wa matibabu wanaweza kulipa kwa matumizi yao ya huduma fulani zinazofadhiliwa na mpango.

Kiasi cha Kupunguzwa: Kiasi ambacho mpokeaji wa bima anapaswa kulipia, kama inavyoelezwa na sera ya bima, kabla ya kampuni ya bima kulipia gharama za matibabu.

Ada za Jumla: Jumla ya ada kamili za shirika kwa gharama za huduma za afya za wagonjwa.

Huduma za Jumla: Huduma ambazo zimechaguliwa kwa mgonjwa, hazifadhiliwi na makampuni ya bima, na tayari zimefanyiwa punguzo na D-HH kutoka kwenye ada za jumla na zinahitaji malipo ya awali, kwa mfano, huduma za urembo.

Huduma za Malipo ya Awali: Huduma ambazo sio za muhimu kimatibabu na zinahitaji malipo kutoka kwa mgonjwa kabla ya kutolewa.

Asiye na Bima: Mgonjwa hana bima au msaada wa mtu mwingine kumsaidia kufikia matakwa ya malipo yake.

Punguzo Lisilo la Bima: Punguzo linatokana na njia ya “uchunguzi wa ada ya Mpango wa Huduma za Afya kwa huduma pamoja na walipaji binafsi” kama inavyoelezwa chini ya kanuni zinazotumika ikitekeleza Sehemu ya 501(r) ya Kanuni za Mapato ya Ndani. Punguzo hili linatumiwa kabla ya kumpa mgonjwa bili na kabla ya kutumia marekebisho yoyote ya msaada wa kifedha. Punguzo hili halitumiwi kwa malipo yoyote ya pamoja, bima ya pamoja, kiasi cha kupunguzwa, malipo ya awali au huduma za pamoja ambazo tayari zinalenga punguzo lolote linalotakiwa, au kwa huduma zilizo kwenye kundi la zisizofadhiliwa na makampuni yote ya bima. Punguzo linahesabiwa kila mwaka na linarekebishwa kama inavyohitajika mwanzoni mwa mwaka wa fedha.

Dartmouth-Hitchcock Health: Kwa ajili ya sera hii Wanachama wa Mfumo wa Dartmouth-Hitchcock Health (D-HH) ni Hospitali ya Alice Peck Day Memorial, Kituo cha Matibabu cha Cheshire, Mt. Ascutney Hospital and Health Centre, New London Hospital, na Visiting Nurse and Hospice for Vermont and New Hampshire (VNH). Hospitali zingine zote huko New Hampshire na Vermont zinachukuliwa kama Vituo Visivyo Wanachama.

Kufikia tarehe 11 Mei 2019, sera hii inatumika kwa Dartmouth-Hitchcock Clinic, Mary Hitchcock Memorial Hospital, Alice Peck Day Memorial Hospital na Cheshire Medical Center.

Kufikia mwezi Mei 2020, sera hii pia itatumika kwenye Hospitali ya New London.

IV. Kauli ya Sera

D-HH inakubali kupokea kutoka kwa wagonjwa wasio na bima, kama malipo yaliyo kamili, kiasi ambacho sio kikubwa kuliko kile ambacho huwa kinatozwa na kupokelewa na D-HH kutoka kwa wagonjwa wenye bima ya afya. D-HH inatumia punguzo lisilo la bima dhidi ya jumla ya tozo kabla kumtoza mgonjwa ambaye ni raia wa Marekani. Punguzo hili halitumiwi kwa malipo yoyote ya pamoja, bima ya pamoja, kiasi cha kupunguzwa, malipo ya awali au huduma za pamoja ambazo tayari zinalenga punguzo lolote linalotakiwa, au kwa huduma zilizo kwenye kundi la zisizofadhiliwa na bima zote. Wagonjwa ambao hawana uraia wa Marekani na wanatafuta huduma zisizo za dharura hawastahili kupokea punguzo lisilo la bima.

Wagonjwa wasio tayari kukiri uraia wao, hawafuzu kupata punguzo lisilo la bima.

<u>501(r) Njia ya kuhesabu Asilimia ya AGB:</u>

Kanuni za IRS chini ya Sehemu ya 1.501(r)-5, Kima cha Ada, unazihitaji hospitali kuhesabu asilimia yao ya “kiasi cha kiujumla kinachotozwa kwa wagonjwa walio na bima” asilimia ya (AGB). Hospitali zinaruhusiwa kutumia njia ya kukagua nyuma ili kuelekeza asilimia ya AGB kwenye madai ya Mpango wa Huduma za Matibabu ada-kwa-huduma pamoja na

watoa bima wote binafsi, au kwa kutumia Mpango wa Huduma za Matibabu tu. Kanuni hizi zinabainisha zaidi kwamba mipango ya bima ya huduma za afya inayosimamiwa na watoa bima wa sekta binafsi chini ya Faida ya Mpango wa Huduma za Matibabu inapaswa kuchukuliwa kama mipango ya watoa bima za afya wa sekta binafsi na siyo Mpango wa Huduma za Matibabu ada-kwa-huduma.

Taasisi za D-HH zilizorejelewa hapo juu zimechagua kuelekeza ukokotoaji wao wa asilimia ya AGB kwa kutumia njia ya kuchunguza nyuma kwa madai ya Mpango wa Huduma za Matibabu ada-kwa-huduma pamoja na watoa bima wote wa sekta binafsi. Kwa kutumia kipindi cha mwaka hadi mwaka cha miezi 12 mfululizo, ada za jumla kwa Mpango wa Huduma za Matibabu ada-kwa-huduma na walipaji wote binafsi zinajumuishwa, pamoja na mapato ya huduma za wagonjwa kwa makundi haya haya. Asilimia ya AGB inahesabiwa kama ifuatavyo:

$$\text{Asilimia ya Kiasi cha Makusanyo} = \frac{\text{Jumla ya Mpango wa Huduma za Matibabu FFS \& Mapato ya Huduma za Wagonjwa ya Walipaji Binafsi}}{\text{Jumla ya Mpango wa Huduma za Matibabu FFS \& Jumla ya Tozo za Walipaji Binafsi}}$$

Asilimia ya AGB = 100% - Asilimia ya Kiasi cha Makusanyo

V. Marejeleo - N/A

Mmiliki Husika:	Idara ya Fedha ya Kampuni	**Anwani:**	Kimberly Mender
Imeidhinishwa Na:	Bodi ya Wadhamini; Afisa Mkuu - Fedha; Ofisi ya Usaidizi wa Sera - Sera za Shirika Tu; Mender, Kimberly; Naimie, Tina	**# ya Toleo**	6
Tarehe ya Sasa ya Idhinisho:	19/11/2019	**Kitambulisho cha Hati ya Zamani:**	RMD 0081
Tarehe ambayo Sera itaanza Kutumika:	19/11/2019		
Sera & Taratibu Husika:	Usaidizi wa Kifedha kwa Sera ya Huduma za Afya		
Misaada ya Kazi Husika:			